# Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb
# Shule ya Watoto Inayofadhiliwa na Bahati Nasibu
# Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara

## Bahati Nasibu ya Mapema

### Ni umri gani unaohitajika kwa mwanafunzi kujisali katika Pre-K?

Ili kustahiki mwaka wa masomo wa 2020-2021, tarehe ya kuzaliwa ya mtoto wako inapaswa kuwa kati ya tarehe zifuatazo: Septemba 2, 2015-Septemba 1, 2016.

### Ikiwa mtoto wangu anaishi nje ya eneo la mahudhurio la Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb (DCSD), je anastahiki kushiriki katika mpango wa Pre-K?

Hapana. Ikiwa anwani yako ya nyumbani haiko katika Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb, haustahiki kushiriki. Ikiwa huna uhakika ikiwa anwani yako iko katika DCSD, nenda kwenye http://www.dekalbschoolsga.net/operations/school-locator/ ili kuthibitisha.

### Je, ninaruhusiwa kuomba zaidi ya shule moja?

Hapana. Unaweza kujisajili katika shule ya wilaya, ikiwezekana, au shule yako ya nyumbani. Ukichagua kujisajili katika shule ya wilaya na ukose kuchaguliwa, utawekwa moja kwa moja kwenye orodha ya kusubiri. Baada ya wiki ya kwanza ya shule, ikiwa kuna nafasi katika shule yako ya nyumbani, unakaribishwa kujisajili kwa nafasi katika shule yako ya nyumbani.

### Je, ikiwa mtoto wangu anastahiki Shule ya Watoto, lakini hakushiriki katika mpango wa Pre-K uliofadhiliwa na jimbo, bado anastahiki kujisajili katika Pre-K?

Ili kustahiki mwaka wa masomo wa 2020-2021 kama mwanafunzi wa Shule ya mapema ya Watoto, mtoto wako lazima awe na Mpango Binafsi wa Elimu (IEP) ambao unatambua hitaji la kuchukua muda wao wa Shule ya mtoto katika darasa jumuishi la Pre-K.

### Je, mtoto wangu amefunzwa kutumia poti ili kujisajili katika Pre-K?

Mtoto wako anatarajiwa kuweza kufanya kazi za kujishughulikia kama vile kujivalisha nguo, kujivua nguo, na mahitaji ya choo. Watoto wanapaswa kufunzwa kutumia poti kabla ya kuingia Pre-K. Wazazi wataitwa iwapo tukio litatokea na watahitajika kuja shuleni kumbadilisha mtoto wao. Wanafunzi hawapaswi kuvaa nepi za kuvuta shuleni isipokuwa iwe imeangaziwa kama sehemu ya Mpango Binafsi wa Elimu (IEP) au mpango wa 504 na mtoto ako katika darasa shirikishi, ili aweze kusaidiwa na mwalimu/msaidizi wa mahitaji maalum.

### Kama mfanyakazi wa DCSD ninapokea usajili otomatiki katika bahati nasibu ya Pre-K?

Hapana. Kama mfanyakazi wa DCSD lazima upitie mchakato ule mmoja wa bahati nasibu kama kila mtu. Hata hivyo, kuna masharti mahsusi kabla ya wafanyakazi kuingia katika bahati nasibu ya Pre-K. Tafadhali wasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako au Ofisi ya Early Childhood kwa*DeKalb Pre-K Lottery Employee Participation Memo*.

### Mtoto wangu amekuwa na IEP na kwa sasa hajaandikishwa katika DCSD. Je, atasalia katika shule ya mtoto wangu kama atateuliwa katika bahati nasibu?

Ikiwa mwombaji mwenye Mpango Binafsi wa sasa wa Elimu (IEP) amechaguliwa kuhudhuria darasa la kawaida la elimu la Pre-K la Bright from the Start (BFTS), huenda mwombaji

akahamishwa kwa darasa shiriki la BFTS kulingana na mahitaji ya kibinafsi ya mwanafunzi. **KUMBUKA:** Shule za jimbo hazina madarasa shirikishi ya BFTS

Mtoto wangu wa miaka mitatu ana IEP inayoendelea *na amesajiliwa tayari katika darasa la mahitaji ya kipekee la DSCD,* je, ninapaswa kumsajili kwa Pre-K?

Hapana. Ikiwa mtoto mtoto wako ana IEP inayoendelea na kwa sasa anahudumiwa katika darasa la watoto wa umri wa miaka mitatu ataandikishwa katika Pre-K kulingana na mahitaji yake ya IEP.

Je, ni hati gani zinazohitajika kwa mwanafunzi kuomba bahati nasibu ya Pre-K?

Thibitisho la kuzaliwa, thibitisho la mzazi wa kisheria (ikiwa jina la mzazi/mlezi haliko kwenye cheti cha kuzaliwa), thibitisho la kitambulisho cha mzazi/mlezi, na thibitisho la makazi. Orodha kamili ya hati zote zinazohitajika, na maelezo ya kina, yanaweza kupatikana kwa kubofya kwenye kichupo cha "Mchakato wa Bahati nasibu" kwenye kiungo kifuatacho https://www.dekalbschoolsga.org/pre-k/

## Baada ya Bahati Nasibu

Mtoto wangu alichaguliwa katika bahati nasibu, nifanye nini sasa?

Hatua yako inayofuata ni kukubali nafasi hiyo na kubeba barua yako ya kukubaliwa uliyopokea pamoja na hati zilizosalia za usajili katika shule yako tarehe iliyoashiriwa ili ukamilishe usajili wako. *Hatua hii inayofuata ni muhimu kukamilisha katika muda uliopewa au unaweza kupoteza nafasi yako kwa mtu mwingine kwenye orodha ya wanaosubiri.*

Itakuwa aje iwapo mtoto wangu hakuchaguliwa katika bahati nasibu?

Mwanafunzi yeyote ambaye hakuchaguliwa kwa nafasi ya bahati nasibu huwekwa kiotomatiki kwenye orodha ya wanaosubiri. Mfumo hupanga wanafunzi kulingana na nambari kwenye orodha ya wanaosubiri na kwa kawaida barua huzalishwa ili kumwarifu mzazi kuhusu nafasi yao kwenye orodha ya wanaosubiri. Kwa kuwa nafasi zinaweza kukataliwa au kubatilishwa, mfumo huzalisha barua ya kukubaliwa kwa mtu anayefuata kwenye orodha ya wanaosubiri. Kwa wakati huo, utahitajika kukamilisha hatua zifuatazo ili kulinda nafasi yako ya bahati nasibu.

Itakuwa aje kama siwezi kutoa fomu 3231 ya Chanjo ya Afya kabla ya tarehe iliyoashiriwa ya usajili kwenye barua ya kukubaliwa?

Sera ya DCSD inasema kwamba ni lazima mtoto awe na fomu 3231 ya Chanjo ya Afya kwenye faili ndani ya siku 30 za mtoto kuanza shule au tarehe ya muda kuisha. Kama hazitapatikana, mtoto hataweza kurejea darasani bila fomu au uthibitisho la miadi. Mtoto hataweza kurudi baada ya miadi bila fomu iliyosasishwa. Iwapo mtoto hatakuwa shuleni kwa siku 10 mtawalia kwa sababu ya fomu hii kutopeanwa, nafasi ya mtoto katika Pre-K itabatilishwa.

Itakuwa aje kama siwezi kutoa fomu 3300 ya Kusikia, Kuona, Meno na Lishe kabla ya tarehe iliyoashiriwa ya usajili kwenye barua ya kukubaliwa?

Sera ya DCSD inasema kwamba ni lazima mtoto awe na fomu kwenye faili ndani ya siku 90 za mtoto kuanza shule au tarehe ya muda kuisha. Kama hazitapatikana, mtoto hataweza kurejea darasani ambayo inaweza kusababisha mtoto kupoteza nafasi yake katika mpango huu.

## Itakuwa aje ikiwa mtoto wangu ni lazima atumie dawa zilizoagizwa na daktari mchana?

Baada ya kumsajili mtoto wako kwa nafasi yake ya Pre-K, hakikisha umeleta maelezo ya dawa. Shule itakuwa na mtu wa kuongea na wewe kuhusu fomu za dawa na taratibu za kutumia dawa hizo zilizoagizwa na daktari.

## Ni nini kitafanyika ikiwa mtoto wangu hatakuwepo siku ya kwanza ya shule?

Wanafunzi wote walioteuliwa wa bahati nasibu wanatarajiwa kuwepo na kuhesabika siku ya kwanza ya shule. Ikiwa mtoto wako hatahudhuria kabla ya saa 10:00 AM siku ya kwanza ya shule, nafasi yake itabatilishwa na kupewa mtu anayefuata kwenye orodha ya wanaosubiri.

## Je, kuna sera ya mahudhurio kwa wanafunzi wa Pre-K?

Ndiyo, wanafunzi wanatarajiwa kuhudhuria siku nzima ya mafunzo katika kipindi cha mwaka mzima wa shule. Watoto wasiohudhuria darasa au wanaochelewa kwa siku kumi mtawalia bila sababu za kimatibabu, lazima waondolewe darasani kulingana na maagizo ya jimbo. Kwa kuongezea, wanafunzi wanaoonyesha mtindo wa kuchelewa kila wakati au kutoka mapema wanaweza kupoteza nafasi yao na wataelekezwa kwa mshauri /au mhudumu wa jamii.

## Je, kuna mahitaji yoyote ya kushiriki kwa wazazi wa Pre-K?

Ndiyo, wazazi wanatarajiwa kushiriki katika mikutano yote iliyopangwa na makongamano ya wazazi angalau mara mbili kwa mwaka na mara zaidi ikihitajika. (Shughuli hizi zitadumu takriban saa moja).

## Itakuwa aje nikiwa na swali lolote ambalo halijashughulikiwa katika FAQ?

Jihisi huru kuwasiliana na Ofisi ya Early Childhood @ 678.676.0147